035713655

**KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS**

# KCPE

516004

# KISWAHILI
# SEHEMU YA KWANZA
# LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

    **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
    **JINA LAKO**
    **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano:**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
    A. waraka
    B. barua maalum
    C. barua ya kiofisi
    D. Barua rasmi

    Jibu sahihi ni **D**

    **Katika karatasi ya majibu:**

    **2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

**GEUZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15 . Kwa kila nafasi umepewa maneno manne hapo chini. Chagua neno lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Lisemwalo lipo na kama ____1____ li njiani laja. ____2____siku ya Jumamosi mwendo wa saa kumi ____3____ pale miamba wawili wa soka walipokutana kusakata ____4____. Refa alipuliza ____5____ iliyowasisimua mashabiki waliokuwa wengi ajabu katika uwanja. ____6____ wa nyayo. Mechi ____7____kwa kasi huku kila timu ____8____ kufunga ____9____ bao la kuwaweka kifua mbele mapema.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. haliko | B. lipo | C. halipo | D. halimo |
| 2. | A. Tulikuwa | B. Ilikuwa | C. Yalikuwa | D. Ulikuwa |
| 3. | A. macheo | B. asubuhi | C. adhuhuri | D. alasiri |
| 4. | A. kabumbu | B. vumba | C. kabambe | D. kivumbi |
| 5. | A. kipenga | B. firimbi | C. putangi | D. moto |
| 6. | A. marufuku | B. mbaya | C. maarufu | D. nzuri |
| 7. | A. ilianza | B. zilianza | C. yalianza | D. walianza |
| 8. | A. tujitahidi | B. wakijitahidi | C. yakijitahidi | D. ikijitahidi |
| 9. | A. au | B. kama | C. angalau | D. angaa |

Kadri ____10____ kukua, ndivyo hulka ilivyozidi ____11____. ____12____ alionywa mara kwa mara na mama yake ____13____ kitu kutoka kua mgeni, yeye ____14____. Hatimaye kitumbua ____15____ kikaingia mchanga. Ilimbidi kukatisha masomo yake kwa muda.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. alizidi | B. alivyozidi | C. alikua | D. alichagua |
| 11. | A. kuvutia | B. kuimarika | C. kuzorota | D. kumstawisha |
| 12. | A. Ijapokuwa | B. Ikiwa | C. Kama | D. Sembuse |
| 13. | A. asiwapokee | B. asipokee | C. asiuze | D. awapokee |
| 14. | A. hakusikitika | B. hakufundisha | C. alisikia | D. hakusikia |
| 15. | A. lake | B. yake | C. chake | D. wake |

***Kutoka swali 16 - 30, chagua jibu mwafaka kulingana na maagizo uliyopewa;***

**16.** Mstari mmoja wa ubeti wa shairi huitwa
A. mizani B. kibwagizo
C. ubeti D. mshororo

**17.** Wanafunzi wameenda ________ kucheza.
A. uwanjani B. kwa uwanja
C. katika uwanjani D. ndani ya uwanja

**18.** Chagua methali isiyoonyesha ushirikiani
A. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo
B. Kamba ya mbali haifungi kuni
C. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
D. Jifya moja haliinjiki chungu

**19.** Mwikali amekula machungwa mengi <u>mno</u>. Neno lililopigiwa mstari ni
A. kihusishi B. kitenzi
C. kielezi D. kivumishi

**20.** Maneno yaliyo katika ngeli ya U - I ni
A. ulemavu, wema, wakati
B. mwembe, mifupa, mpamba
C. ubao, ubavu, ufizi
D. ugali, uji, ugoro

**21.** Ni sentensi ipi iliyotumia kivumishi cha pekee?
A. Firimbi ya refarii ilipatikana uwanjani
B. Mpira wangu ulipotea jana
C. Magari haya mengi yanatutatiza
D. Magunia yeyote yatakayonunuliwa yasiuzwe

**22.** Fanicha kwa mfano meza, viti, madawati na makabati huitwa
A. samani B. sanamu
C. zamani D. viwanda

**23.** Chagua ugonjwa ambao si wa kuambukizana
A. Homa B. Pepopunda
C. Ukambi D. Mafua

**24.** Tunasema friji
A. hicho hicho B. hilo hilo
C. hii hii D. hayo hayo

**25.** Baraza la wazee ni nomino ya
A. makundi B. jamii
C. pekee D. dhahania

**26.** Mtu anapotiwa mbaroni na kupelekwa kwenye kituo cha polisi huitwa
A. mshtakiwa B. mfungwa
C. mshukiwa D. mwizi

**27.** *Kanusha sentensi ifuatayo;*
Niliend a nikampata akilala.
A. Nilienda nikampata amelala.
B. Sikuenda na sikumkuta akilala.
C. Nilienda na nilimkuta amelala.
D. Sikwenda wala sikumpata amelala.

**28.** Gurudumu lilipasuka ________ kisha kimya kikatanda.
A. paa, jii B. buu, zi
C. puu, jii D. buum, jii

**29.** ***Andika wingi wa sentensi hii;***
Mtoto wangu alimpiga mtotowe.
A. Watoto wangu walimpiga mtotowe.
B. Watoto wetu waliwapiga watotonu.
C. Watoto wenu waliwapiga watoto yao.
D. Watoto wako waliwapiga watotowe.

**30.** ***'Hana mbele wala nyuma,'*** ina maana
A. maskini hohehahe
B. tajiri wa kupindukia
C. yeye ni mlafi
D. yeye ni kiwete

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40;***

Safari iling'oa nanga. Kila jambo lilikuwa shwari. Hapakuwa na shari yoyote. Chombo kilianza kuyanyoa mawingu kwa haiba yake. Mtambo uliendelea kunguruma vizuri kinyume cha matarajio ya limbukeni asiye na siri. Ardhi ya nchi walikwisha iacha na hawakuwa na haja nayo tena, wakapaa kama ndege angani. Labda patokee dharura ambayo itamlazimu rubani arejee tena ardhini, jambo ambalo wakati huo halikuonekana kuwa rahisi.

Masumbuko alimwuliza mwenziwe aliyeketi naye karibu yaliyosemwa. Alifahamishwa kuwa maelezo ya akina dada hao huwa ya kawaida kabla ndege haijaondoka naye hakumjibu. Kwani hakutaka kuonekana mjinga zaidi ya jinsi alivyojichukulia. Watu waliosalia pale uwanjani waliona ndege hiyo ikipaa kama kipanga apaaye angani kwa mbawa zake. Ulikuwa mwendo wa saa moja unusu usiku lakini kwa sababu ya taa nyingi zilizozagaza mwanga pale uwanjani ungeweza kufikiria ulikuwa mchana wa jua la mtikati. Masumbuko aliendelea kumwambia Maulana huku safari yao ikishika kasi. Alifurahia fursa hiyo aliyedhania ingefaa kupewa kiongozi wa nchi au mgeni yeyote

mashuhuri.

Baada ya ndege kutokomea angani na kuchukua usawa uliostahili, ilitua ikaanza kuongezeka kasi zaidi. Wahudumu wakaanza kuwagawia abiria vyakula ili wayatulize matumbo yao nao wanywaji wa mvinyo wakapata fursa ya kuyatuliza makoo yao.

Masumbuko alipewa chakula chake. Alijaribu kula kwa uma, kisu na kijiko jinsi walivyokuwa wakifanya katika kambi ya mazoezi uwanjani Kasarani. Lakini pengine kwa sababu ya raha kupindukia au kutojiamini ama ulimbukeni alishindwa kabisa kuvitumia vifaa vya kulia. Kila alipojaribu kula kwa kutumia kijiko, uma na kisu mambo yalimwendea mrama. Chakula kilikuwa kikidondokadondoka chini na kama si chakula basi ni uma, kijiko au kisu.

Masumbuko hakutaka kujifedhehesha zaidi. Aliamua kula kwa mikono yake aliyoipangusa kwa kitambaa cheupe kilichochemshwa katika majimoto ya ndimu. Aliona ni heri ainyofoe minofu ya kuku kwa kutumia vidole vya mikono yake kuliko kujiabisha. Uamuzi huo ulimfanya yeye na wenziwe kadhaa wale kwa mikono baada ya kuziweka kando zana za kulia chakula.

Abiria wengine walishangazwa na vijana hao kwa kuamua kula kwa mikono yao. Walipomaliza kula, masumbuko aliagizia sharubati ya maembe akaletewa. Wenziwe pia waliagiza vinywaji chaguo lao wakanywa wakashiba wakashukuru. Bahati aliyeketi karibu na Masumbuko naye hakuzembea kwani aliagiza Sharubati hiyo baada ya kumwambia mhudumu mmoja kuwa angependa kuletewa kinywaji sawa na alichokuwa akinywa mzungu aliyeketi mbele yake. Mara Radhia akafikiwa na mhudumu mwingine alimkumbusha aletewe sharubati kama aliyokuwa akiinywa ndugu aliyeketi mbele yake.

Mhudumu huyo hakusita kutekeleza wajibu wake. Alikuwa amevizoea visanga sampuli hiyo vilivyokuwa kawaida kukumbana navyo akiwa kazini. Alienda mekoni na baada ya dakika mbili tatu hivi akarejea akiwa amebeba glasi ya plastiki iliyojaa sharubati ya karakara. Katika dakika za kuhesabu, Masumbuko akaanza kusinzia kisha usingizi ukamparamia na kumteka nyara.

Kufumba na kufumbua, alijipata amezama katika bahari ya Luja akiongeza na kumteka nyara Rades jijini Tunis. Alikuwa akichuana na wanariadha wengine mbioni. Kila alipojaribu kupiga hatua wapinzani wake walizidisha kasi. Alijihisi kudhulumiwa akaanza kupunguza mwendo.

Alipotaka kuacha kukimbia alizisikia sauti alizozifahamu tosha zikimhimiza kwa kusema. "Masumbuko, hili ni fursa yako kujiokoa na ukiwa ufukara na kuwaokoa wenziwe katu usiiache ikuponyoke." Maneno hayo yaliuatua moyo wake. Aliyauma meno kwa uchungu na dhiki kama duma aliyemwona mchopozi wa wanawe, akafyatuka kama risasi na kwa sekunde kadhaa akawafikia na kuwapiku waliomtangulia. Alipokuwa akivikwa taji ya ubingwa alihisi kisulisuli akayafumbua macho yake huku akifikiri kuwa kazi kilikuwa kimetawala kwa weusi kaniki hasa kisha akasalimu amri na alipogutuka alisikia sauti ya rubani ikisema maneno fulani kwa Kiingereza.

31. Chombo kilianza kuyanyoa mawingu kwa haiba yake. Kinachozungumziwa hapa ni
A. meli B. gari
C. mtambo D. ndege

32. Kinyume cha **limbukeni** ni
A. mjusi B. mjuzi
C. mjinga D. msafiri

33. Rubani ni kwa ndege ilhali meli ni kwa
A. nahodha B. dereva
C. hamali D. kandawala

34. Ni nini ilisababisha mwangaza mkubwa pale uwanjani?
A. Taa za ndege B. Ilikua jioni
C. Taa zilizoenea kote D. Kulikuwa mchana

35. Masumbuko aklifurahia safari ile kwa sababu
A. ilikuwa mara yake ya kwanza ndegeni
B. alikuwa akienda ziara rasmi
C. alialikwa na rais wa nchi jirani
D. aliteuliwa kuwa balozi

36. Masumbuko alishindwa kuvitumia kijiko, uma na kisu. Hii ni kutokana na
A. raha kupindukia
B. kutojiamini sana
C. ulimbukeni wake
D. aliambiwa asivitumie

37. Mzungu alikuwa akinywa sharubati ya
A. limau B. karakara
C. machungwa D. maembe

38. Visanga mwandishi anavyozungumzia hapa ni kama vile
A. kusumbuliwa na wateja wengi
B. kutojua kutumia vifaa vya kulia
C. kuagiza sharubati badala ya chai
D. kuagiza chakula au kinywaji hakijui jina

39. Kuzama katika bahari ya Luja ni
A. kuogelea baharini B. kuanguka majini
C. kuwa na ndoto D. kufikiria sana

40. Kichwa kinachofaa habari hii ni
A. Masumbuko na rubani
B. Vituko katika ndege
C. Safari ya mbali
D. Ndoto ya ajabu

***Soma kifungu kifuatacho na kisha uyajibu maswali 41 - 50 kwa usahihi;***

Janga la Ukimwi ni mojawapo ya maradhi ambayo yamempa binadamu usumbufu usiokuwa na kifani. Tangu janga hili livamie taifa letu juhudi za mchwa zimefanyika kukumbana nao bila mafanikio mwafaka.

Wafadhili nao wamechangia pakubwa kwa kumwaga fedha zao kuukabili ukongo huu katika viwango mbalimbali. Uhamasisho wa kutosha umefanywa kiasi cha kwamba asilimia sabini na tano kwa mia ya umma yaufahamu na kuujua ugonjwa huu.

Nawaomba washikadau wote washirikiane kuona ya kwamba dawa za kupunguza makali yake zimesambazwa katika kila gatuzi kwenye hospitali na zahanati zote za umma na kibinafsi.

Wahakikishe kuwa wale walioathiriwa na hawawezi kupata lishe ya hata siku moja wangesaidiwa kufanya hivyo. **Viokote** wote wameachwa nyuma na wapenzi au wavyele wao, wamepangiwa namna wanavyoweza kushughulikiwa.

Wahenga hawakukosea waliponena mpigwa na wengi hajui amuumizaye. Nawe ukiwa mtu wa kujifanya kijongoo au koo asiyetosheka, chunga usije ukajilaumu mwenyewe. Aidha mwiba wa kujichoma hauna pole.

---

**41.** Je, madaktari wamefaulu katika kuvumbua dawa ya kutibu ugonjwa wa Ukimwi kwa sasa?
A. Karibu watafaulu
B. La! Hasha
C. Walifaulu kitambo
D. Ndiyo! Walifaulu

**42.** Kulingana na kifungu hiki, ni watu wangapi wamehamasishwa kuhusu ugonjwa huu?
A. Wengi  B. Wachache
C. Wote  D. Sabini na watatu

**43.** Ni neno lipi halifai katika kundi hili?
A. Fedhea  B. Fedha
C. Hela  D. Pesa

**44.** Wafadhili wamemwaga fedha nyingi. Hii ina maana kuwa na
A. hazikutoza
B. zilifujwa
C. ziliwekwa benki
D. zilitumiwa

**45.** Kulingana na habari hii, ni kweli kusema
A. wafadhili walitoa pesa
B. waja walihamasishwa
C. robo ya watu walifahamishwa
D. robo tatu ya watu walipata mafunzo

**46.** Neno **viokote** limepigwa mstari. Lina maana ya
A. walemavu  B. mzazi
C. mwananchi  D. mayatima

**47.** ***"Mpigwa na wengi hajui amuumizaye."*** Hii ni
A. methali  B. semi
C. tashbihi  D. nahau

**48.** Ni neno lipi halina maana sawa na ugonjwa?
A. Ukongo  B. Uwele
C. Maradhi  D. Uele

**49.** ***"Mwiba wa kujichoma hauna pole."*** Hii ni methali inayotumiwa
A. kuonya mtu
B. kumshtumu mtu
C. kumlilia mtu
D. kumpongeza mtu

**50.** Kichwa mwafaka cha habari hii ni
A. Wafadhili  B. Ukimwi
C. Viokote  D. Wazazi

***Andika insha ya kusisimua inayoanza kwa maneno yafuatayo;***

Matone machache ya mvua yalionekana yakianguka ardhini. Mengine makubwa mazito yalifuatia. Hatimaye ..............................................................................................................